msingi Majengo na Magereza na shule za sekondari za Kazima na Lwanzari zote za

msaada huo huku akisema serikali inaendelea na juhudi za kuhakikisha inamaliza

madawati.

Baadhi ya wanafunzi walisema msaada huo

HABARI LEO UK 7.

# Ulega aahidi kutatua mgogoro wananchi, ranchi ya Kitengule

**Na Diana Deus, Karagwe**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amewahakikishia wananchi na wawekezaji wilayani Karagwe kushughulikia kwa haraka mgogoro wa kitalu namba moja kinachopakana na Kijiji cha Mushabaiguru, Kata ya Kihanga ili kuondoa migogoro ya mifugo kati ya wananchi na wawekezaji walioko maeneo ya ranchi ya Kitengule.

Alitoa kauli hiyo katika mkutano wa hadhara na wananchi wa Kata ya Kihanga, wilayani Karagwe alipotembelea miradi mbalimbali na kusikiliza kero za wananchi katika maeneo hayo ukiwemo mgogoro huo wa Ranchi ya Kitengule, Kitalu namba moja ambao umekuwepo tangu kipindi cha nyuma na kupelekea sintofahamu kati ya wakulima, wafugaji na mwekezaji.

Diwani wa Kata ya Kihanga, Rwamuhangi Rwamugata alimuomba Ulega kuangalia namna ya kuwabadilishia mpaka walau kuondoa adha ya mifugo inayovuka mipaka na kuingia kwa mwekezaji na kusababisha migogoro isiyoisha jambo ambalo linakwamisha shughuli za maendeleo katika kata hiyo.

Akizungumzia mgogoro huo, Ulega alikiri kuwa ugomvi baina ya mwekezaji wa ranchi ya Kitengule kutokana na mifugo kuingiliana na mashamba ya wananchi na kuahidi kuwa suala hilo amelichukua kwa uzito na hatua zitachukuliwa kwa haraka ili usalama uendelee kuwepo wilayani humo.

Katika mkutano wa hadhara na wananchi aliwasisitizia ufugaji wenye tija ili kupata maziwa ya kutosha kutokana na wilaya hiyo kupata mwekezaji ambaye amejenga kiwanda cha kusindika maziwa kitakachowanufaisha wafugaji wengi wa wilaya hiyo.

Katibu Tawala Mkoa wa Kagera, Toba Nguvila alisema serikali inaendelea kushirikiana na wafugaji na kuendelea kuwajengea uwezo ikiwemo kuwapa elimu ya ufugaji bora wenye tija.

CamScanner

## ...a Tume ya Vyuo Vikuu

wazisajili
hatimaye
anufaisha
mawazo


waliyotoa
ika banda
kutambua
ubunifu.
izwa kwa
wananchi
alisema,
ishaji wa
biashara.
anchi na
a kufika
masuala
ashara na
wa upana



...ya

a ndani,
uboresha
a moto,"

mbali
o ujenzi
aendelea
vilaya na
ni moja,
a uliopita
pata sh.
e kutoka
a ujenzi
sha wodi
wa ndani
ntoto.
, alisema
2022/23,
oni 400
ambavyo
vituo na
kutolewa.
vaka huu;
gewa sh.
nua vifaa
00 na sh.
ya ujenzi
a afya.



# Vijana BBT waanza kuonja faida ya kazi

**Na MWANDISHI WETU**

VIJANA waliojiunga na programu ya BBT Mifugo wanaoendelea na mafunzo ya unenepeshaji katika kituo cha Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) Kikulula, wameanza kuonja matunda ya mafunzo yao baada ya kuuza ng'ombe 310 waliowanenepesha kwa muda wa miezi mitatu.

Hayo yalifahamika wakati wa ziara ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyoifanya katika kituo hicho kilichopo wilayani Karagwe, mkoani Kagera.

Akizungumza kwa niaba ya vijana wenzake, Salum Husidicheki, alisema hadi sasa wameshauza ng'ombe 310, awamu ya kwanza waliuza ng'ombe 150 na ya pili ng'ombe 160.

"Wastani wa bei tulizofanikiwa kuuza ng'ombe wetu sio chini ya laki sita na nusu (650,000), na katika mauzo hayo faida kwa kila ng'ombe haipungui elfu tisini (90,000)," alisema.

Pia, alimshukuru Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwawezesha kupata fursa hiyo ya mafunzo kwa sababu wanaamini kupitia mafunzo hayo wataweza kuwa na ujuzi wa ufugaji wa kibiashara na kukuza kipato chao.

**WAZIRI ULEGA**

Naye, Waziri wa Mifugo na Uvuvi,

> **Wastani wa bei tulizofanikiwa kuuza ng'ombe wetu sio chini ya laki sita na nusu (650,000), na katika mauzo hayo faida kwa kila ng'ombe haipungui elfu tisini (90,000).**
>
> Salum Husidicheki

Abdallah Ulega aliwapongeza vijana hao kwa hatua hiyo ya kuanza kuuza mifugo kwani inaashiria kuwa, tayari wameshaanza kupata ujuzi na watakapomaliza mafunzo yao wanaweza kuendesha maisha yao kupitia biashara hiyo ya mifugo.

Alisema maono na dira ya Rais, Dk. Samia ni kuifanya hiyo programu ya BBT inaenea nchi nzima na vijana waingie katika uzalishaji mali kupitia rasilimali zilizopo hapa nchini.